**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI TARIME**

# YAH: MAELEKEZO YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2024 KATIKA HALMASHAURI YA MJI TARIME

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Mji Tarime kwa mamlaka aliyopewa chini ya kanuni ya **9** ya ***Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji Tangazo la Serikali na.574 la tarehe 12/7/2024,*** anautaarifu Umma kuwa:-

(i).Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Mji Tarime utafanyika siku ya **tarehe 27 Novemba 2024.**

(ii) Uandikishaji wa orodha ya wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi huo utafanyika kuanzia tarehe **11 hadi 20 Oktoba 2024** katika Mitaa yote **81** kwa maana kila Mtaa utakuwa na Kituo kimoja na vituo vya uandikishaji vitafunguliwa kuanzia saa **2:00 asubuhi** na kufungwa saa **12:00 jioni** katika kipindi chote cha uandikishaji (Orodha ya Vituo husika imeambatishwa kwa rejea).



CamScanner

(iii). Uchaguzi utafanyikia katika vituo ambavyo vitatumika kuandikisha orodha ya wapiga kura **tarehe 27 Novemba 2024** kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi **saa 10:00 jioni**

(iv). Wakazi wote wenye sifa za kupiga kura ikiwa ni pamoja na raia wa Tanzania ambao ni wakazi wa Mitaa husika na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea wanahimizwa kushiriki katika uchaguzi.

(v). Wakazi wenye umri wa miaka ishirini na moja na kuendelea wanaotaka kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa wanahimizwa kuchukua fomu za kugombea zitakazopatikana kwenye **Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi** (Ofisi ya Mtaa)

(vi). Fomu za kuomba kugombea nafasi za uongozi (uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa) zitaanza kutolewa kuanzia tarehe **1 Novemba 2024 (saa 1:30 asubuhi hadi saa 10:00 jioni)** na tarehe ya mwisho ya urejeshaji wa fomu hizo ni tarehe **7 Novemba 2024.**

(vii). Uteuzi wa wagombea utafanyika siku ya **tarehe 8 Novemba 2024** na majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa yatabandikwa sehemu ya matangazo ya uchaguzi katika Mtaa.



CamScanner

(viii). Pingamizi kuhusu uteuzi zitapaswa kuwasilishwa **tarehe 8 na 9 Novemba 2024** na uamuzi wa pingamizi kuhusu uteuzi utatolewa kati ya **tarehe 8 na 10 Novemba 2024..**

(ix). Rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi zitawasilishwa kati ya **tarehe 10 na 13 Novemba 2024** na uamuzi wa Kamati ya Rufaa utatolewa kati ya **tarehe 10 na 13 Novemba 2024.**

(x). Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe **20 hadi 26 Novemba 2024.**

***"Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, jitokeze kushiriki Uchaguzi"***

Maelekezo haya yametolewa tarehe 26 Septemba 2024.

Gimbana E. Ntavyo
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**
**TARIME MJI**

**Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze kushiriki Uchaguzi.**

CamScanner

| VITUO VYA KUANDIKISHIA WAPIGA KURA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| SN | KATA | MTAA | ENEO /KITUO |
| 1 | Sabasaba | Makire | Eneo la wazi |
| 2 | Sabasaba | Kimusi | Eneo la wazi |
| 3 | Sabasaba | Chomete | Zahanati ya Chomete |
| 4 | Sabasaba | Songambele A | Eneo la Wazi |
| 5 | Sabasaba | Songambele B | Eneo la wazi |
| 6 | Sabasaba | Nyarusahi | Ofisi ya mtaa |
| 7 | Sabasaba | Sabasaba | S/M Sabasaba |
| 8 | Sabasaba | Kibasa | Eneo la wazi |
| 9 | Sabasaba | Samartani | Eneo La Wazi |
| 10 | Sabasaba | Iganana | Ofisi ya Kata (vibanda vya Serengeti) |
| 11 | Sabasaba | Nyangai | Eneo la wazi |
| 12 | Sabasaba | Serengeti | Eneo la wazi |
| 13 | Turwa | Buguti | Eneo la wazi |
| 14 | Turwa | Rebu Shuleni | Rebu Sekondari |
| 15 | Turwa | Kokehogoma | Eneo la wazi |
| 16 | Turwa | Gimenya | Ikohi S/M |
| 17 | Turwa | Rebu Senta | Rebu S/M |
| 18 | Turwa | Mkuyuni | Turwa sekondari |
| 19 | Turwa | Kebikiri | Ofisi ya Kata |
| 20 | Turwa | Uwanja/Ndege | Ikolo sekondari |
| 21 | Ketare | Nyamaisana | Ofisi ya Mtaa |
| 22 | Ketare | Kibumaye | Kituo cha Afya Kibumaye |
| 23 | Ketare | Kedeli | S/M Kedeli |
| 24 | Ketare | Nyamiobo | Chekechea |
| 25 | Ketare | Ketatukya | S/M Mtingiro |
| 26 | Ketare | Nyangasara | Eneo la wazi |
| 27 | Ketare | Binagi | Eneo la wazi |
| 28 | Ketare | Kwigoronto | Sekondari Nkongore |
| 29 | Ketare | Maruru Senta | Stooni |
| 30 | Ketare | Nyamasamore | Chekechea |
| 31 | Ketare | Mogabiri Senta | Ofisi ya Mtaa |
| 32 | Ketare | Butirya | S/M Ntabulo |
| 33 | Ketare | Nsomba | Eneo la Wazi |
| 34 | Nkende | Nkende Shuleni | Gicheri Sekondari |
| 35 | Nkende | Taramoroni | S/M Taramroni |
| 36 | Nkende | Kinyambi | Nkende sekondari |
| 37 | Nkende | Rembirwi | S/M Ncharo |
| 38 | Nkende | Regoryo | S/M Regoryo |
| 39 | Nkende | Ketare | Eneo la Wazi |
| 40 | Nkende | Nyamiobo | S/M St Luka |
| 41 | Nkende | Romoli | Eneo la wazi |
| 42 | Nkende | Kwibanga | Ofisi ya mtaa |
| 43 | Nkende | Itebe | Ofisi ya mtaa |

CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| 44 | Nkende | Nyamitembe | Eneo la wazi |
| 45 | Nkende | Magena Senta | Ofisi ya Mtaa |
| 46 | Nkende | Magena Shuleni | S/M Magena |
| 47 | Nkende | Kirumi | S/M Nyamwino |
| 48 | Nkende | Kumuturu | S/M Kemahiri |
| 49 | Nkende | Kogesenda | Eneo la wazi |
| 50 | Nyamisangura | Ronsoti | Zahanati ya Ronsoti |
| 51 | Nyamisangura | Msati | Nyamisangura Sekondari |
| 52 | Nyamisangura | Bugosi | S/M Bugosi |
| 53 | Nyamisangura | Msatihighway | Turwa s/m |
| 54 | Nyamisangura | Starehe | Ofisi Ya Mtaa |
| 55 | Nyamisangura | Mwangaza | S/M Nyamisangura |
| 56 | Bomani | Buhemba | S/S Bomani |
| 57 | Bomani | Bomani | Eneo inapojengwa nyumba ya Mkurugenzi |
| 58 | Bomani | Biambwi | Chuo Cha Ualimu |
| 59 | Bomani | Mawasiliano | Ujenzi |
| 60 | Bomani | Magereza | Ofisi ya Kata |
| 61 | Bomani | NHC | S/M Tarime |
| 62 | Bomani | Anglikana | Eneo la wazi |
| 63 | Nyandoto | Masurura | Zahanati ya Masurura |
| 64 | Nyandoto | Nyagesese | S/S Nyagesese |
| 65 | Nyandoto | Nyakehenene | S/M Gamasara |
| 66 | Nyandoto | Nyasebe | Eneo la wazi |
| 67 | Nyandoto | Mnagusi | Angel Sekondari |
| 68 | Nyandoto | Itununo | Ofisi ya Kata |
| 69 | Nyandoto | Kemoge | St Jude |
| 70 | Nyandoto | Nguku | Ofisi ya Mtaa |
| 71 | Nyandoto | Nyamonkanga | Nyandoto Sekondari |
| 72 | Nyandoto | Nyansurura | S/M Nyansurura |
| 73 | Nyandoto | Biambwi | Ofisi ya Maji |
| 74 | Kenyamanyori | Makao | Ofisi ya Mtaa |
| 75 | Kenyamanyori | Ronga | Eneo la Wazi |
| 76 | Kenyamanyori | Kogete | Ofisi ya Mtaa |
| 77 | Kenyamanyori | Mwibari | S/M Mwibari |
| 78 | Kenyamanyori | Nyametembe | S/M Nyametembe |
| 79 | Kenyamanyori | Tagota | Ofisi ya Mtaa |
| 80 | Kenyamanyori | Kebaga | S/M Mtahuru |
| 81 | Kenyamanyori | Chira | Ofisi Ya Mtaa |

CamScanner